
# JARIDA la eGA

## Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 6 | Oktoba-Disemba 2023

# UBADILISHANAJI TAARIFA KIDIJITALI WAIMARIKA




✓ Taasisi 109 zaunganishwa GovESB

✓ Mifumo 117 Imesajiliwa

# Yaliyomo kwenye Jarida


3 Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

4 Salamu za Mwaka Mpya

5 Ubadilishanaji taarifa kidijitali Serikalini waendelea kuimarika

7 Kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kufanyika Februari jijini Arusha

8 e-GA na Mzumbe kushirikiana katika tafiti na ubunifu

9 Mifumo ya Kielektroniki yazuia upotevu wa mapato ya Serikali

10 Maafisa TEHAMA Kilimo washauriwa kuzingatia Sheria ya Serikali Mtandao

11 Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA watakiwa kukabiliana na mabadiliko ya Teknolojia

12 Tuko tayari Kushirikiana na Sekta binafsi : e-GA

13 Taasisi za Umma zabainisha faida za mfumo wa e-Mikutano


15 Miaka 62 ya Uhuru: e-Ga yaziunganisha Taasisi za Hakijinai Kidigitali

16 Fahamu Kuhusu Chat AI

17 e-GA kuendelea kuwajengea uwezo maafisa TEHAMA Serikalini

18 Sekta ya Usafirishaji yashauriwa kubuni mifumo ya TEHAMA yenye tija

19 Habari Katika Picha



# Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibu katika toleo la sita la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Katika jarida hili utasoma kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka, kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi na uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao.

Pia utafahamu kuhusu utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosaidia kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za utoaji wa huduma kwa Umma.

Vile Vile, katika Jarida hili utaweza kufahamu jitihada zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa sheria ya Serikali Mtandao namba 10 ya 2019 .

Toleo hili ni mfululizo wa habari zinahusu jitahada za e-GA katika kuratibu,kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma ili kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika Jarida hili ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza

Nakutakia usomaji mwema na Heri ya Mwaka Mpya 2024

Mhandisi Benedict B. Ndomba

**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# Salamu za Mwaka Mpya

**KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO(e-GA)**

Kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), tunapenda kuwatakia nyote Heri ya Mwaka Mpya 2024. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake na mwongozo wake uliotuwezesha kufikia mafanikio mbalimbali mwaka uliopita.

Mwaka huu mpya wa 2024 unaleta fursa mpya, changamoto, na matumaini mapya. Tupo tayari kushirikiana na wadau wetu katika kuleta mabadiliko chanya na kuboresha huduma za serikali kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Tunatoa wito kwa wizara, wakala, Idara za Serikali, taasisi na mashirika ya umma, sekta binafsi na wadau wote kujitokeza kwa wingi kushirikiana nasi katika kufanikisha malengo yetu ya kuleta mapinduzi ya kidigitali na kufanya huduma za serikali kuwa bora zaidi.

Tunapenda kuwashukuru kwa ushirikiano wenu wa karibu mwaka uliopita na tunatarajia kuendelea kushirikiana kwa karibu zaidi mwaka huu mpya wa 2024.

Tunawakaribisha wote katika Kikao Kazi cha Nne (4) cha Mwaka cha Serikali Mtandao kitakachofanyika tarehe 6 – 8 Februari 2024, katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano (AICC) jijini Arusha. Katika kikao hicho, tutakuwa na fursa ya kujadili kwa pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma na kuimarisha ushirikiano wetu ili kuhakikisha utoaji wa huduma serikalini kidijitali unaimarika.

Heri ya Mwaka Mpya 2024! Tushirikiane kwa pamoja katika safari hii ya kuijenga Serikali Kidijitali.




**Dkt. Mussa Kissaka**
**Mwenyekiti ya Bodi ya Wakurugenzi**




# UBADILISHANAJI TAARIFA KIDIJITALI SERIKALINI WAENDELEA KUIMARIKA

> ◊• Kampuni 1,496 za wakala wa forodha (CFA)pamoja na makampuni ya watunza shehena 246 zinatumia Mfumo wa TeSWS.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba, amesema kuwa, jumla ya taasisi za umma 109 zimeunganishwa katika Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji taarifa Serikalini ujulikanao kama Government Enterprises Service Bus (GovESB), na tayari mifumo ya TEHAMA 117 imesajiliwa katika mfumo huo.

Mfumo wa GovESB, ni mfumo wa kielektroniki unaounganisha mifumo ya TEHAMA ya taasisi za umma iweze kusomana na kubadilishana taarifa kwa usalama, ili kupunguza urudufu wa mifumo, kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Akizungumza katika mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika tarehe 22 Desemba, 2023 jijini Dodoma, Ndomba alisema kuwa, miongoni mwa taasisi zilizojiunga na mfumo huo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Leseni za Biashara (BRELLA) na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

"Mfumo wa GovESB, umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuzingatia kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuanzisha na kuendesha Mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA Serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa", alifafanua Ndomba.

Aliongeza kuwa, sambamba na utekelezaji wa takwa la kisheria pia, ujenzi wa mfumo huo ni utekelezaji wa agizo la Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, la kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inaunganishwa na kubadilishana taarifa.

"Mfumo huu umeleta mafanikio katika sekta mbalimbali ikiwemo ya sheria, ambapo taasisi za hakinijnai yaani Mahakama, Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS), zimejiunga na zinabadilishana taarifa kupitia GovESB na hivyo kusaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, uwazi pamoja na utoaji haki kwa wananchi kwa wakati", alisisitiza Ndomba.

Sanjari na hilo, Ndomba alibainisha kuwa, e-GA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Wizara ya Fedha, imesanifu na kujenga Mfumo wa Pamoja wa Kielekroniki wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS).

Alisema kwamba, Mfumo wa TeSWS ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini – MKUMBI (Blueprint), ili kuwezesha wafanyabiashara kukamilisha maombi ya vibali na maandalizi ya malipo ya kodi za forodha kidijitali, bila kulazimika kufika

kwenye ofisi zinazohusika.

"Mfumo wa TeSWS unaruhusu wadau wa biashara na wasafirishaji kuwasilisha mara moja tu kwenye mfumo taarifa za kiforodha na shehena zinazoingia na kutoka nchini, pamoja na zile zinazopita nchini kwenda nchi jirani ambapo kila mdau anayehusika ataziona na kuzifanyia kazi kwenye mfumo" alieleza Ndomba.

Aliongeza kuwa, mfumo wa TeSWS una awamu tatu ambapo awamu ya kwanza inahusu moduli za taratibu za forodha 'Customs Procedures' na zile za taasisi za Udhibiti na Ukaguzi, na Malipo ya Huduma na tayari inatumika kwa Bandari ya Dar Es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, ambapo kampuni za wakala wa forodha (CFA) 1,496 pamoja na makampuni ya watunza shehena 246 zinatumia mfumo huu.

Awamu ya pili imeanza kutumika na inahusu moduli za taratibu za ujio wa meli na uondoshaji wa shehena maeneo ya forodha 'Cargo Management', na awamu ya tatu inahusu moduli za taratibu nyingine ndogondogo za forodha ndani ya TRA, TPA, Posta na Viwanja vya Ndege na sasa ipo katika hatua ya majaribio.

Kwa upande wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya mifumo ya TEHAMA ya Serikali na ya Sekta binafsi, Ndomba alisema kuwa, ubadilishanaji wa taarifa kati ya sekta hizo, unawezeshwa kadiri ya mahitaji yanavyojitokeza.

"Mfumo wa malipo ya Serikali (GePG) umeunganishwa na Benki zote nchini pamoja na Kampuni zote za Simu za Mikononi, ili kuwezesha huduma ya malipo ya Serikali kupitia simu za mikononi pia, Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi (Government Mobile Platform -mGov) umeunganishwa na mifumo ya kampuni zote za simu nchini, na kuwezesha kutoa huduma za Serikali, kwa njia ya simu za mkononi", alifafanua Ndomba na kuongeza kuwa,

"Ili kuhakikisha taasisi nyingi zaidi zinajiunga na mfumo wa GovESB na kubadilishana taarifa kupitia mfumo huo, tunaendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na taasisi za umma ambapo kati ya Agosti na Novemba 2023, tumefanya vikao na taasisi 55 na sisi tupo tayari muda wowote kuziwezesha taasisi za umma zinazohitaji kujiunga na GoVESB ili ziweze kubaadilishana taarifa".



> "Mfumo wa GovESB, umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuzingatia kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuanzisha na kuendesha Mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA Serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa"
>
> **Mhandisi Ndomba**



**Mkurugenzi Mkuu e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba (wa kwanza kushoto) akieleza kuhusu kuimarika kwa ubadilishanaji taarifa miongoni mwa mifumo ya taasisisi za umma wakati wa Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika tarehe 22/12/2023 katika ofisi za e-GA Makao Makuu zilizopo Mtumba, jijini Dodoma**

# KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO KUFANYIKA FEBRUARI JIJINI ARUSHA




Washiriki wa kikao kazi cha tatu (2023) cha serikali mtandao wakisikiliza kwa umakini mada zilizowasilishwa wakati wa kikao kazi hicho jijini Arusha kilichoandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), inatarajia kufanya kikao kazi cha nne (4) cha Serikali Mtandao Februari 6 hadi 8, mwaka huu katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Akizungumza ofisini kwake jijini Dodoma, Meneja Mawasiliano wa e-GA Bi. Subira Kaswaga amesema, lengo la kikao kazi hicho ni kuwakutanisha wadau wa Serikali Mtandao kutoka katika taasisi na mashirika mbalimbali ya umma, ili kujadili jitihada mbalimbali za utekelezaji wa Serikali Mtandao na kuweka mikakati itakayosaidia kukuza na kuimarisha Serikali Mtandao nchini.

Subira amesema kuwa, kikao hicho kitaongozwa na kauli mbiu isemayo "Uzingatiaji wa Sheria, Sera, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji Salama wa Taarifa".

"Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijitali ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma, lakini pia ili hili liweze kutokea ni lazima tuwe na mifumo ambayo imetengenezwa kwa kuzingatia Sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao", amesema Subira.

Ameongeza kuwa, takriban wadau 1,000 wa Serikali Mtandao kutoka katika mashirika na taasisi mbalimbali ya umma wanatarajiwa kushiriki kikao hicho wakiwemo Maafisa Masuuli, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA, Maafisa TEHAMA na watumiaji wengine wa mifumo ya TEHAMA.

Aidha, Subira amesema kuwa, katika kikao hicho mada mbalimbali zinazohusu Serikali Mtandao zitawasilishwa sambamba na kupata taarifa ya utekelezaji wa maazimio 12 yaliyofikiwa katika kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao kilichonyika Februari mwaka jana.

"Mwaka jana tulifanya kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao na kuweka maazimio 12 ambayo yaliwekwa na washiriki wa kikao hicho, hivyo mwaka huu tutawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo ni wakati mzuri kwa washiriki kufahamu yale waliyokubaliana na kufahamu utekelezaji wake", amefananua Subira.

Aidha, Subira ametoa rai kwa wadau wote wa Serikali Mtandao nchini kujitokeza kwa wingi kushiriki katika kikao kazi hicho na kujisajili kupitia mfumo wa mafunzo na semina (TSMS) unaopatikana kwa kikoa cha www.tsms.ega.go.tz.

"Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijitali ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma, lakini pia ili hili liweze kutokea ni lazima tuwe na mifumo ambayo imetengenezwa kwa kuzingatia Sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao."



Bi. Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano wa e-GA



# e-GA NA MZUMBE KUSHIRIKIANA KATIKA UTAFITI NA UBUNIFU

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Chuo Kikuu Mzumbe, zimesaini hati ya makubaliano (MOU) ya ushirikiano katika masuala ya elimu, utafiti, na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ikiwa ni hatua inayolenga kuimarisha na kukuza tasnia ya TEHAMA ili kuboresha jitihada za Serikali Mtandao sambamba na kuimarisha uhusiano uliopo baina ya taasisi hizo.

Hafla ya utiaji saini wa makubaliano hayo ilifanyika tarehe 17 Oktoba, 2023 katika ofisi za Chuo Kikuu Mzumbe mkoani Morogoro, na kushuhudiwa na baadhi ya watumishi wa taasisi zote mbili pamoja na waandishi wa habari.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Uwezeshaji e-GA, CPA. Salum Mussa, alisema kuwa makubaliano hayo yanalenga kuongeza tija katika kukuza na kuimarisha tasnia ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na kutoa fursa kwa wanafunzi wa tasnia hiyo wa Chuo Kikuu Mzumbe, kujifunza kwa vitendo kupitia program maalum inayotolewa na e-GA katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GovRIDC).

“Pamoja na fursa hiyo kwa wanafunzi, pia ushirikiano wetu na Chuo Kikuu Mzumbe utaimarika zaidi na tunatarajia bunifu nyingi za TEHAMA zitaibuliwa kupitia Kituo chetu cha Utafitifi na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao, kwakuwa tutapata nafasi ya kushirikiana na wataalamu katika tafiti na bunifu mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Mzumbe”, alisema Bw. Salum.

Alifafanua kuwa, Mamlaka imedhamiria kuwaleta wataalamu na watafiti mahiri katika masuala ya TEHAMA kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, ikiwa ni pamoja na Madaktari na Maprofesa wa masuala ya TEHAMA, ili kushirikiana nao kwenye miradi ya bunifu inayozalishwa katika kituo hicho, ambapo wataalamu hao wataweza kutoa ushauri wa namna ya kutatua changamoto mbalimbali ili kuwa na Serikali Mtandao yenye tija.

Naye, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Profesa William Mwegoha, alisema kuwa makubaliano hayo yanaweka msisitizo mkubwa kwenye masuala ya ufundishaji na utafiti ili kuhakikisha wanafunzi wa TEHAMA katika chuo hicho wanajengewa uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka kwa maendeleo ya taifa letu.

“Tunaangazia kuboresha jinsi tunavyotoa elimu kwa wanafunzi wetu wa fani ya TEHAMA, kwa kuwa ushirikiano huu utasaidia kuonesha maeneo ambayo tunatakiwa kuweka msisitizo au kuboresha zaidi ili kuwa na wataalamu wazuri kwenye eneo la TEHAMA, lakini pia itasaidia chuo kuwa na programu zaidi za elimu kwa njia ya mtandao.,” alisema Profesa Mwagoha.

Profesa Magoha alibainisha kuwa, utafiti utakuwa eneo muhimu la ushirikiano kati ya Chuo Kikuu Mzumbe na e-GA, ambapo Watafiti kutoka e-GA watashirikiana na wenzao wa chuo hicho katika kutatua changamoto za kiteknolojia, na kubuni mifumo ya TEHAMA inayoweza kutumika Serikalini ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa umma.



Mkurugenzi wa Huduma za Uwezeshaji e-GA, CPA. Salum Mussa (Kushoto) na Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Profesa William Mwegoha (Kulia) wakisaini hati ya makubaliano



# MIFUMO YA KIELEKTRONIKI YAZUIA UPOTEVU WA MAPATO YA SERIKALI

## Makabidhiano ya Mfumo GPSA Intergrated Management Information System' (GIMIS)

Matumizi sahihi na salama ya mifumo ya kieletroniki Serikalini, yametajwa kuwa suluhisho la kudumu katika kuziba mianya ya upotevu wa rasilimali za serikali ikiwemo mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali nchini.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Fedha Mh. Dkt Mwigulu Nchemba, wakati akipokea na kuzindua Mfumo wa Kieletroni wa Kuratibu Ununuzi wa Mafuta Serikalini, ujulikanao kama 'GPSA Intergrated Management Information System' (GIMIS), kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh.George Simbachawene, katika hafla iliyofanyika tarehe 21 Oktoba, 2023 jijini Dodoma.

Alisema kuwa, matumizi ya mifumo imara ya kielektroniki yanasaidia kuondoa mianya ya upotevu wa rasilimali za Serikali na kudhibiti watumishi wasio waadilifu, kwakuwa malipo yote ya serikali yatalipwa kupitia njia sahihi na salama katika taasisi husika.

"Tukifanya kazi kupitia mifumo ya kielektroniki tunapunguza makosa mengi ya kibinadamu, hivyo matumizi sahihi ya mifumo hii yatatuwezesha kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu ikiwa ni pamoja na eneo la ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya serikali", alifafanua Dkt.Mwigulu.

Akieleza kuhusu mfumo huo Dkt. Mwigulu alisema kuwa, mfumo wa GIMIS unatumiwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), ambapo kwa sasa majukumu yote ya Wakala yanatekelezwa kupitia mfumo huo ambao umesaidia kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, Dkt. Mwigulu aliielekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kuhakikisha inaunganisha mfumo wa Manunuzi Kielektroni (NeST) na mfumo wa GIMIS kwa kuwa, mfumo huo unatumiwa na Wizara, Mashirika ya Umma, Wakala, Ofisi za Mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini katika kupata huduma za GPSA.

> **"Mfumo wa GIMIS umesanifiwa na kujengwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA)."**
>
> Dkt Mwigulu Nchemba
> Waziri wa Fedha

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mh. George Simbachawene alisema kuwa, lengo la mfumo huo ni kurahisisha utendaji kazi wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), katika uuzaji wa mafuta Serikalini, ili kuweka uwazi na kutunza kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika kila taasisi ya umma.

Alisema kuwa, hadi kufikia Oktoba 2023, zaidi ya taasisi nunuzi 7070 zinatumia mfumo huo ambapo, taarifa za matumizi ya mafuta kwa kila taasisi zinatunzwa katika mfumo huo na kusaidia katika uandaaji na usimamizi wa mipango ya bajeti ya ofisi, pamoja na udhibiti wa matumizi sahihi ya mafuta kwa taasisi za umma.

"Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha matumizi sahihi ya mafuta kwa taasisi za umma na kuokoa fedha zilizokuwa zikipotea kutokana na kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi za matumizi ya mafuta", alisisitiza.

Aliongeza kuwa, kupitia mfumo huo, Serikali inaweza kufahamu kiasi cha mafuta yaliyotumika na yaliyobaki, magari yaliyopatiwa mafuta, muda, mahali na tarehe na hivyo kuziwezesha taasisi husika kuweza kudhibiti matumizi ya mafuta ikiwa ni pamoja na kuondoa udanganyifu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu.

Aidha, Mh. Simbachawene alisema kuwa, katika kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuunganisha mifumo ya TEHAMA Serikalini ili iweze kuwasiliana na kubadilishana taarifa Wizara yake kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao tayari imeunganisha mfumo wa GIMIS na GoVESB.

"Tayari tumekwishaunganishwa mfumo huu wa GIMIS kwenye Mfumo Mkuu wa Serikali wa kuwezesha Mifumo Kubadilishana Taarifa ujulikanao kama Government Enterprses Service Bus (GovESB), na umeshaanza kubadilishana taarifa na mifumo ya baadhi ya taasisi za umma kama vile Mfumo wa Kukusanya Mapato ya Serikali (GePG) pamoja na mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Taasisi (ERMS).

Mfumo wa GIMIS umesanifiwa na kujengwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).


UZINDUZI WA MFUMO WA GIMIS



Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw.George Bagomwa (Kulia),akiwasilisha mada katika kikao kazi cha Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo

# MAAFISA TEHAMA KILIMO WASHAURIWA KUZINGATIA SHERIA YA SERIKALI MTANDAO

Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, wametakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao, katika kusanifu miradi ya TEHAMA ili kuhakikisha inaleta tija katika sekta ya kilimo.

Wito huo ulitolewa tarehe 20 Desemba, 2023 na Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw.George Bagomwa, wakati akiwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini, kwenye kikao kazi cha Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA wa taasisi zilizo chini ya Wizara kilichofanyika mkoani Iringa.

> "Ni vema tukafuata matakwa ya sheria ya Serikali Mtandao, kanuni zake, viwango pamoja na miongozo ili mradi wowote wa TEHAMA mtakauanzisha uweze kuleta manufaa kwa wakulima nchini"
>
> Bw. George Bagomwa.
> Afisa TEHAMA,e-GA

Alisema kuwa, uzingatiaji wa Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika uanzishwaji wa miradi ya TEHAMA, utasaidia kutengeneza miradi yenye tija katika sekta ya kilimo.

"Ni vema tukafuata matakwa ya sheria ya Serikali Mtandao, kanuni zake, viwango pamoja na miongozo ili mradi wowote wa TEHAMA mtakauanzisha uweze kuleta manufaa kwa wakulima nchini", alisema Bw. Bagomwa.

Aidha, alifafanua kuwa ikiwi sheria na miongozo ya Serikali Mtandao itazingatiwa na taasisi zikawasilisha miradi ya TEHAMA e-GA kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo, taasisi hizo zitaweza kupata ushauri wa kitaalamu kutoka e-GA katika hatua za awali za uanzishwaji





Baadhi ya Washiriki wa Kikao kazi cha Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo wakifuatilia mada mbalimbali zilizohusu maendeleo ya TEHAMA katika sekta ya Kilimo.

# WACHAMBUZI WA MIFUMO YA TEHAMA WAASWA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA



Kaimu Meneja wa Ushauri na Uelekezi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi.Joan Valentine akiwasilisha mada wakati wa mafunzo ya siku 6 kwa ajili ya Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA kutoka taasisi mbalimbali za Serikali.

Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA 'Business Analysts' katika taasisi za umma, wametakiwa kuongeza elimu na kupata maarifa mapya mara kwa mara, ili kukabiliana na kasi ya ukuaji wa mabadiliko ya teknolojia mpya zinazoibuka, ikiwemo ujuzi katika uchambuzi wa takwimu pamoja na Akili Bandia (Artificial Inteligence).

Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA 'Business Analysts' katika taasisi za umma, wametakiwa kuongeza elimu na kupata maarifa mapya mara kwa mara, ili kukabiliana na kasi ya ukuaji wa mabadiliko ya teknolojia mpya zinazoibuka, ikiwemo ujuzi katika uchambuzi wa takwimu pamoja na Akili Bandia (Artificial Inteligence).

Wito huo ulitolewa na Kaimu Meneja wa Ushauri na Uelekezi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Joan Valentine, wakati akifungua mafunzo ya siku sita kwa Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA yaliyofanyika tarehe 20 hadi 25 Novemba, 2023 katika ukumbi wa TANAPA, Kambarage Tower jijini Dodoma.

Aidha, Bi. Joan aliwataka Maafisa hao kujifunza stadi mbalimbali ikiwemo teknolojia ya akili bandia na uchambuzi wa takwimu, ili ziwasaidie kupambana na mabadiliko ya teknolojia yanayoibuka duniani mara kwa mara na kuhakikisha teknolojia hizo zinasaidia ukuaji wa taasisi zao.

"Kwa sasa dunia inazungumza kuhusu akili bandia, hivyo wachambuzi wa mifumo lazima muwe na ujuzi wa hizi teknolojia ili kuzisaidia taasisi zenu katika utendaji kazi wa kila siku", alisema Bi.Joan. Vilevile, aliwataka maafisa hao kuona umuhimu wa kujifunza stadi tepe 'soft skills' ili ziweze kuwasaidia katika kupambana na mabadiliko yanayoendelea kutokea katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ulimwengu kote.

"Kwa sasa TEHAMA inatoka kuwa fani saidizi 'supporting tool' hadi kuwa fani wezeshi 'enabling tool' hivyo, mnatakiwa muwe wajuzi zaidi katika sekta ya TEHAMA ili kuzisaidia taasisi zenu kupiga hatua katika utendaji kazi wa kila siku", alisisitiza.

Mratibu wa Mafunzo hayo Bw.Ceaser Mwambani ambaye pia ni Mchambuzi wa Mifumo ya TEHAMA e-GA, alisema kuwa, lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA, katika maeneo ya uchambuzi wa mifumo ya TEHAMA, usimamizi wa miradi ya TEHAMA, miongozo, viwango, ubora na usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini.

"Kupitia mafunzo haya, tunaimani kuwa, washiriki wote hapa watakuwa na uelewa zaidi kuhusu uchambuzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA pamoja na kuweza kutoa mchango mzuri kwenye taasisi zao ili kuwa na miradi yenye tija kwa taifa", alifafanua.

Mafunzo hayo ni muendelezo wa jitihada za Mamlaka ya Serikali Mtandao za kuhakikisha inashirikiana na kuzijengea uwezo taasisi za umma katika kukuza jitihada za Serikali Mtandao.

"Kwa sasa dunia inazungumza kuhusu akili bandia, hivyo wachambuzi wa mifumo lazima muwe na ujuzi wa hizi teknolojia ili kuzisaidia taasisi zenu katika utendaji kazi wa kila siku"

Bi.Joan Valentine
Kaimu Meneja wa Ushauri na Uelekezi

**Washiriki wa mafunzo ya Wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA yaliyofanyika katika Ukumbi wa TANAPA,Kambarage Tower jijini Dodoma.**





# TUKO TAYARI KUSHIRIKIANA NA SEKTA BINAFSI: e-GA

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeahidi kushirikiana na Benki ya NMB ili kuimarisha, kukuza na kuendeleza ujuzi na vipaji kwa vijana wa Kitanzania wabunifu na wale wanaosoma fani ya TEHAMA, katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini, kupitia programu maalum ya mafunzo kwa vitendo inayotolewa na e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC).

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 11 Oktoba, 2023, na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba, wakati wa kikao cha pamoja kati ya e-GA na benki ya NMB, kilichofanyika katika Makao Makuu ya ofisi za e-GA jijini Dodoma, kwa lengo la kujadili namna taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya teknolojia.

Maeneo hayo ni pamoja na utafiti, matumizi ya teknolojia za kisasa, kuvumbua vipaji na kuviendelea kwa wavijana wabunifu wa Kitanzania, pamoja na kutoa fursa kwa vijana wavumbuzi na wabunifu ikiwa ni sehemu ya kuendeleza sekta ya TEHAMA nchini.

Ushirikiano huo unatarajiwa kuongeza na kukuza fursa za ajira kwa vijana sambamba na kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na sekta binafsi kwenye eneo la TEHAMA, alisema Ndomba.

"e-GA imekuwa ikishirikiana na Vyuo Vikuu mbalimbali nchini katika kuwapata vijana wenye ujuzi, hivyo makubaliano haya kati ya e-GA na NMB ni muendelezo wa ushirikiano mzuri uliopo kati ya e-GA na wadau mbalimbali wa TEHAMA", alifafanua Ndomba.

Aliongeza kuwa, katika kikao hicho taasisi hizo zimekubaliana kushirikiana na kuandaa mkataba wa makubaliano (MOU) ambapo baada ya kukamilika kwa mkataba huo, pande zote mbili zitakutana na kujadiliana namna ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

"e-GA imekuwa ikiwatengeneza vijana wanaoshiriki programu maalum ya mafunzo kwa vitendo pamoja na utaratibu wa kujitolewa (interns and volunteering) kupitia kituo chetu cha utafiti na ubunifu, kwa kuwajengea uwezo zaidi ili kwenda sambamba na soko la ajira pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoibuka kila siku", alisema Ndomba.

Aidha, Ndomba aliishukuru Benki ya NMB kwa kuona umuhimu wa kutengeneza wataalamu wazawa wa TEHAMA kupitia programu hiyo na kuahidi kuwa, e-GA ipo tayari kushirikiana na benki nyingine zenye dhamira ya kuijenga Tanzania ya kidijitali katika sekta zote za serikali na binafsi.

Naye Meneja eGovRIDC Dkt. Jaha Mvulla alisema, e-GA ipo tayari kushirikiana na Benki ya NMB katika maeneo mbalimbali yanayolenga kukuza matumizi ya TEHAMA nchini ikiwemo eneo la rasilimali za miundombinu na vifaa vya TEHAMA vya kufanyia mazoezi na majaribio, ubunifu hasa maeneo ya teknolojia mpya, kujenga uwezo na uzoefu kwa vijana, mafunzo kwa vitendo, utafiti na machapisho, maonesho, mashindano mbalimbali ya kidigitali kwa ajili ya kuvumbua vipaji, na maeneo mengine yanayohusiana na jitihada za Serikali Mtandao na teknolojia za kifedha.

"e-GA ipo tayari kufanya kazi na NMB kupitia programu maalumu ya mafunzo kwa vitendo inayoendeshwa na eGovRIDC, ili kuchochea ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka duniani ikiwemo Akili Bandia (AI), Machine Learning, Blockchain na matumizi yake kama vile kujenga ulewa wa teknolojia kama za Digital Currency na FinTech, Utengenezaji wa mifumo (System Development) kwa ajili ya kutatua changamoto zetu nchini na usalama mtandaoni (Cyber Security)", alisema Dkt.Jaha.

Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu- Kituo cha Taaluma NMB Bi. Joanitha Rwegasira alisema kuwa, Benki ya NMB imeandaa programu hiyo ili kuongeza idadi ya vijana wabobezi kwenye masuala ya TEHAMA watakaofanya kazi katika sekta za umma na binafsi kwa lengo la kukuza taifa la kidijitali.

Programu hiyo itasaidia kufanya majaribio ya teknolojia mpya zinazoibuka ikiwemo Sarafu ya mtandaoni na kutoa suluhu kwenye maeneo mbalimbali yenye changamoto katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi ikiwemo matishio ya usalama mtandaoni, ubunifu wa mifumo n.k, alisema Rwegasira

Aidha, aliishukuru Mamlaka kwa kuonyesha utayari wa kushirikiana na NMB na kwamba watatumia fursa hiyo katika kuhakikisha wanaboresha huduma za kibenki hususani huduma zinazotolewa kidijitali.



# TAASISI ZA UMMA ZAELEZA FAIDA ZA MFUMO WA e-MIKUTANO

Viongozi na watendaji wa taasisi mbalimbali za umma, wameeleza kuwa, mfumo wa uendeshaji wa vikao kidijitali wa e-Mikutano umesaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi zao pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Hayo yameelezwa hivi karibuni wakati wa mahojiano maalum yaliyofanywa na mwandishi wetu katika nyakati tofauti na viongozi hao, alipowatembelea katika ofisi zao.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bw. Masha Mshomba, amesema kuwa mfumo wa e-Mikutano umekuwa na msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya NSSF, kwakuwa umerahisisha vikao vingi kufanyika kwa wakati na hivyo kuokoa muda na gharama za uendeshaji wa ofisi.

"Nakumbuka nilianza kutumia mfumo huu Juni 2022, ambapo tulifanya mkutano na wadau wengi wa hifadhi ya jamii, mfumo huu umetuwezesha kufanya mikutano kidigitali, na sasa siyo lazima tukutane ana kwa ana, kwani hata kama wahusika wa mkutano wapo katika mazingira tofauti, kupitia mfumo huu tumeweza kufanya mikutano kwa muda tunaokubaliana mahali popote", alifafanua Bw.Mshomba.

Aliongeza kuwa, pamoja na kuokoa muda pia, mfumo wa e-Mikutano umesaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwani watumishi hawalazimiki kusafiri ili kukutana ana kwa ana kwa ajili ya kufanya vikao na hivyo kutumia muda mwingi kutekeleza majukumu yao ya kazi badala ya kutumia muda huo safarini ili kuhudhuria vikao.

"Mbali na faida zitokanazo na mfumo huu binafsi naipongeze na kuishukuru e-GA, kwani imekuwa ikitoa ushirikiano wa karibu sana katika kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye mfumo huu na mifumo mingine ya TEHAMA, na ndiyo maana hatuna wasiwasi juu ya ufanisi wa mfumo huu kwakuwa e-GA imekuwa ikitatua changamoto zinazojitokeza wakati wowote na kwa wakati", alisema Bw. Mshoma.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) Bw.Abdul-Razack Badru amesema kuwa, mfumo wa e-Mikutano umekuwa msaada mkubwa kwenye taaisi hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa wakati na ufanisi zaidi.

"Tunafanya mikutano na watumishi wote wa HESLB mara mbili kwa wiki kupitia mfumo huu wa e-Mikutano, kwa hiyo watumishi wote wanapata nafasi ya kushiriki mikutano hiyo muhimu mahali walipo, mfumo huu umetuondolea gharama za watu kusafiri ili kushiriki mikutano pamoja na kupunguza matumizi ya karatasi", amebainisha Bw.Badru.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TEHAMA na Takwimu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Bw.Leopord Shayo, amesema kuwa tangu taasisi hiyo ianze kutumia mfumo wa e-Mikutano uendeshaji wa vikao umekuwa rahisi na wenye ufanisi.

"Ni mfumo rafiki sana, unaweza ukawa unaendesha gari lakini muda ukifika unapaki pembeni ya barabara na kufungua simu yako na kuhudhuria kikao hivyo hata zile udhuru za watu kutoshiriki vikao zinapungua", alisema Bw.Shayo.

Akieleza kuhusu chimbuko la mfumo huo, Afisa Tehama wa e-GA Bw. Juvenali Tarimo amesema kuwa, mfumo wa e-Mikutano ulibuniwa wakati wa changamoto za janga la Uviko-19 ambapo kulikuwa na ugumu wa kufanya mikusanyiko, hivyo ililazimika kubuniwa kwa mfumo huo ili mikutano na vikao viendelele kufanyika kwa njia ya mtandao.

Bw.Tarimo amebainisha kwamba, mfumo wa e-Mikutano ulianza kutumika rasmi mwezi Mei mwaka 2020 na hadi kufikia Novemba 2023, zaidi ya mikutano 12,290 imeshafanyika kupitia mfumo huo katika taasisi za umma 200 kutoka Tanzania Bara na Visiwani.


Baadhi ya taasisi hizo ni LATRA, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Benki Kuu ya Tanzania (BOT),Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT).

"Mfumo huu ni rafiki sana kwa watumiaji, ili mtumiaji aweze kutumia mfumo huu anapaswa kuwa na (laptop, kishkwambi au simu janja) ili ashiriki mijadala inayoendelea kwenye kikao husika na kuhakikisha vifaa hivyo vina uwezo wa kutumia sauti na video", alifafanua Bw.Tarimo.

Mfumo wa e-Mikutano unapatikana kupitia https://mikutano.gov.go.tz/ pia unaweza kupakua applikesheni ya e-mkikutano kwenye 'Playstore' katika simu janja (smartphone)

"Mfumo huu umetuwezesha kufanya mikutano kidigitali, na sasa siyo lazima tukutane ana kwa ana, kwani hata kama wahusika wa mkutano wapo katika mazingira tofauti, kupitia mfumo huu tumeweza kufanya mikutano kwa muda tunaokubaliana mahali popote."

Bw.Masha Mshomba.
Mkurugenzi Mkuu,
NSSF.






Prof. Elisante Ole Gabriel
Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania

# MIAKA 62 YA UHURU: e-GA YAZIUNGANISHA TAASISI ZA HAKIJINAI KIDIGITALI

Miaka 62 iliyopita, Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka kwa utawala wa kikoloni, na tangu wakati huo, imepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo ambapo tunashuhudia mabadiliko makubwa, hasa katika muktadha wa maendeleo ya kidijitali na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Katika kuadhimisha miaka 62 ya uhuru, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kuweka nguvu katika kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma, kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango, na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kujenga taifa la kidijitali.

Lengo ni kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA yanazingatiwa katika taasisi za umma, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma na kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kidijitali mahali walipo.

Katika kufikia malengo ya kuijenga serikali ya kidijitali, e-GA imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mifumo ya TEHAMA inayolenga kuboresha ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi hizo pamoja na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Miongoni mwa mifumo hiyo ni Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) ambao unaziwezesha Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama, uharaka na kwa gharama nafuu. Mfumo huu umeimarisha mawasiliano kwa njia ya baruapepe kwa Taasisi za Umma, umeongeza usalama wa ubadilishanaji taarifa na una kinga dhidi ya wadukuzi, hivyo ni salama zaidi kwa usiri wa taarifa za Serikali.

Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) ambao umejengwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka Serikalini. Mfumo huu umetengenezwa kwa lengo la kupunguza matumizi ya karatasi, gharama, kurahisisha mawasiliano, kurahisisha mzunguko wa nyaraka na majalada ndani ya Taasisi za Umma, kurahisisha kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Katika kuimarisha mawasiliano kati ya wananchi na serikali, e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetengeneza mfumo wa e-Mrejesho unaowezesha wananchi kuwasilisha maoni, malalamiko, maulizo au pongezi kwenda kwenye taasisi za umma kwa njia ya kidijitali.

Mawasiliano hayo, yanaweza kufanyika kupitia simu za kiganjani kwa kupiga *152*00# na kuchagua namba 9 kisha namba 2 na kuendelea na maelekezo. Vilevile, Mfumo huu unapatikana kupitia (link) ya https.//emrejesho.gov.go.tz na kwa kupakua aplikesheni ya e-Mrejesho kwenye simu janja.

Hii ni baadhi ya mifumo iliyotengenezwa na e-GA na inatumika katika taasisi mbalimbali za umma zikiwemo taasisi zinazohusika na utoaji wa haki.

Pamoja na ujenzi wa mifumo hiyo ambayo huimarisha na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma, e-GA



ubadilishanaji wa taarifa kupitia mfumo wa GoVESB, umerahisisha utendaji kazi wa Mahakama kwa kuongeza ufanisi na uwazi katika mchakato wa utoaji wa haki.


Prof. Elisante Ole Gabriel
Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania




**Katika kuadhimisha miaka 62 ya uhuru, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kuweka nguvu katika kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma, kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango, na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kujenga taifa la kidijitali.**

imetengeneza pia mfumo unaowezesha mifumo ya Serikali kubadilishana taarifa ujulikanao kama Government Enterprises Service Bus (GoVESB).
Mfumo huu, unaiwezesha mifumo ya TEHAMA ya taasisi za umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama, hivyo husaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma pamoja na kuokoa muda kwakuwa taarifa hupatikana kidijitali na kwa wakati.

Hadi sasa, taasisi mbalimbali za umma zinabadilishana taarifa kupitia mfumo wa GoVESB zikiwemo taasisi zinazohusika na masuala ya haki (haki jinai) kama vile Mahakama, Jeshi la Polisi (TPF), Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).
Uunganishwaji wa mifumo ya haki jinai ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kuitaka e-GA kuunganisha mifumo yote ya haki jinai ili iweze kuzungumza na kubadilishana taarifa, kuweka uwazi katika utoaji wa haki kwa wananchi pamoja na kurahisisha utendaji kazi katika taasisi hizo.
Pamoja na maelekezo ya Mhe. Rais, pia ripoti ya Tume ya Hakijinai iliyotolewa Julai mwaka huu, ilipendekeza kutengenezwa kwa mfumo wa TEHAMA utakaoziunganisha taasisi za haki jinai ili kurahisisha uwazi katika mchakato wa utoaji wa haki.
Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania Prof. Elisante Ole Gabriel, anasema Mahakama inabadilishana taarifa na taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
Aidha, Prof. Elisante anabainisha kuwa, ubadilishanaji wa taarifa kupitia mfumo wa GoVESB, umerahisisha utendaji kazi wa Mahakama kwa kuongeza ufanisi na uwazi katika mchakato wa utoaji wa haki.
"Mfumo wa GoVESB umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Mahakama kwakuwa, tunaweza kupata taarifa kwa urahisi kutoka taasisi tulizoingia nazo makubaliano na kuweza kubadilishana taarifa kidijitali, vilevile umesaidia kuongeza ufanisi na uwazi katika kuwahudumia wananchi kwa wakati", anasema Prof. Elisante.
Pamoja na kutengeneza mfumo wa GoVESB na kuziunganisha taasisi za haki-jinai, je Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inafanya jitihada gani nyingine za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika taasi za haki jinai?
Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba anasema kuwa, Mamlaka imetoa computer za kisasa 10 kwa Jeshi la Polisi ikiwa ni mchango wake kwa jeshi hilo, katika kuhakikisha linatumia TEHAMA katika utendaji kazi wake ili kuimarisha utoaji wa haki kwa wananchi kidijitali.
"Pamoja na kuwa tumeunganisha Mifumo ya haki jinai na sasa taasisi hizo zinaweza kuzungumza na kubadilishana taarifa, lakini tuliona ni vyema pia Mamlaka ikachangia computer kwa jeshi letu la polisi, ili kuhakikisha na sisi tunashiriki vema kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika chombo hiki muhimu katika utoaji wa haki", alisema Ndomba.
Ndomba anabainisha kuwa, Computer hizo zilikabidhiwa kwa viongozi wa jeshi la polisi Machi 13, mwaka huu katika Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Kanda ya Dar es Salaam na kuwa, e-GA imekuwa ikishirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma likiwemo Jeshi la Polisi, katika kuhakikisha matumizi ya Teknolojia yanarahisisha utendaji kazi wa Taasisi na utoaji wa huduma kwa umma.
"Teknolojia hurahisisha mchakato wa utoaji wa haki na sisi e-GA tukaona ni vizuri kuchangia kwa kutoa kompyuta hizi ili zirahisishe mchakato wa haki jinai katika Jeshi la Polisi", anasema Ndomba.
Ikumbukwe kuwa, kabla ya kuanza kutumia mfumo wa GoVESB, taasisi zililazimika kuwasilisha maombi ya kupata taarifa kwa njia ya barua katika taasisi husika, na hivyo kuchukua muda mrefu kupata taarifa hizo, jambo lililochangia kupunguza ufanisi katika utendaji wa kazi na utoaji wa haki.
Vilevile, changamoto nyingine ilikuwa ni utofauti wa utaratibu wa kupata taarifa kutoka taasisi moja hadi nyingine, kwani kila taasisi ina utaratibu wake wa ndani wa kupata na kutoa taarifa na pia, baadhi ya taasisi utaratibu huo hubadilika mara kwa mara, lakini kupitia GoVESB changamoto hizo zimetatuliwa na sasa taasisi zote za hakijinai zinapata taarifa kwa wakati.
Mfumo wa GoVESB umesaidia kuokoa muda wa kuwahudumia wananchi, lakini pia kupunguza gharama za kutengeneza mifumo midogo midogo ya kuunganisha na taasisi nyingine.
"Pamoja na faida nyingi zitokanazo na mfumo wa GoVESB, si taasisi zote zimejiunga na mfumo huu, jitihada zinaendelea kutambua na kuwezesha taasisi zote zinazotakiwa au kuhitaji kubadilishana taarifa na taasisi nyingine zinajiunga na GoVESB", anasema Ndomba.
Mfumo wa GoVESB umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuzingatia kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuanzisha na kuendesha Mfumo unaowezesha Mifumo ya TEHAMA Serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa.




# FAHAMU KUHUSU Chat AI

Akili Bandia maarufu kama ***'Artificial Intelligence (AI)'*** ni teknolojia inayolenga kujenga mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi kwa kufanana na akili ya binadamu.

Teknolojia hii, ni miongoni mwa teknolojia mpya zinazoibuka kwa sasa duniani na kushika kasi ya matumizi kwenye sekta mbalimbali, zikiwemo sekta za biashara, afya, elimu n.k. Lengo la teknolojia hii ni kutoa uwezo wa kufikiri, kujifunza, kutatua matatizo, na kufanya maamuzi kwa njia inayofanana sawa na ubongo wa binadamu.

Programu za AI zinaweza kufundishwa kutambua vitu kama picha au sauti, hii inaweza kutumika katika maeneo kama utambuzi wa vitu, sura, maandiko au hotuba, Mfumo unaotumia AI pia inaweza kufundishwa kuelewa na kutoa majibu kwa lugha ya asili, kama vile mazungumzo ya binadamu.

Sasa nakupa habari njema rafiki! Kituo cha Utafiti na Ubunifu cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGOVRIDC) , kimebuni na kujenga programu ya kompyuta ya Akili Bandia au Artificial Intelligence iitwayo ChatAI (Chat AI), inayoweza kuwasiliana na binadamu kupitia ujumbe wa maandishi au sauti na kutoa habari au msaada kulingana na kile ambacho mtumiaji anasema au kuandika.

Subiri sasa nikusimulie vizuri, program hii imewezeshwa kutumia lugha yetu pendwa ya taifa yaani Kiswahili, hivyo usiwe na wasiwasi kila Mtanzania anapaswa kufurahia na kutumia hivyo, kazi ni kwako sasa. Pia ChatAI inaweza kupokea Sauti au maandishi nayo ikakujuza kwa sauti au maandishi yaani ( Text to Speech and Speech to Text)

Unajiuliza ChatAI huyu anafanyaje kazi? Ni rahisi sana hebu fikiria kama msaidizi wa kawaida wa dijiti ambaye unaweza kuchati naye, kama vile unavyotuma ujumbe kwa rafiki, lakini rafiki huyu wa dijiti amefanyiwa programu ya kutoa habari za Serikali na kusaidia katika kazi za usaidizi kwa wateja.

Ahaa! Umeelewa sasa eeh! Lengo kuu la program hii ni kufanya huduma za Serikali ziweze kupatikana zaidi na rafiki kwa watumiaji, na hapa ile dhamira ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ya kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha huduma za Serikali zinawafikia wananchi mahali walipo inatimia kupitia ChatAI huyu.

Kingine muhimu unapaswa kujua ni kuwa; ChatAI huyu anaweza kueleza huduma mbalimbali za Serikali na kujibu maswali ambayo watu wanaweza kuwa nayo kuhusu huduma hizo. Hii inamanufaa kwa raia ambao wanataka kuelewa huduma zinazotolewa na Serikali lakini hawajui mahali pa kupata habari sahihi na sasa ChatAI huyu anakujibu maswali yote.

Si hivyo tu rafiki,nikujuze sasa; ChatAI hii inaweza pia kubadilisha ujumbe wa maandishi kuwa sauti, hapa namaanisha kuwa inaweza kusoma majibu kwa watumiaji, kwa sauti kwa watu ambao wanapendelea kusikiliza badala ya kusoma ( Text to Speech and Speech to Text). Umeona ee sasa! ChatAI ni msaidizi wa dijiti wa habari za Serikali na yupo tayari kwa watumiaji, wenye uwezo wa kusiliana kupitia maandishi na hata kubadilisha maandishi kuwa sauti kwa urahisi zaidi.

Kwa taaifa zaidi tembelea:

www.ubunifu.ega.go.tz



**Makamu Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Dkt. Faustine Ndugulile (Kulia), akipewa maelezo ya jinsi program ya ChatAI inavyofanya kazi na Meneja wa Kituo cha kituo cha Utafiti,Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao Dkt. Jaha Mvulla.**

# e-GA KUENDELEA KUWAJENGEA UWEZO MAAFISA TEHAMA SERIKALINI



Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imesema kuwa itaendeleza utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Maafisa TEHAMA wa taasisi za umma ili kuwajengea uwezo na kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu Serikali Mtandao.

Kauli hiyo ilitolewa Novemba 25 jijini Dodoma na Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA e-GA Bw.Ricco Boma, wakati akifunga mafunzo ya siku sita kwa Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka katika taasisi mbalimbali za umma, yaliyotolewa na e-GA.
"Utoaji wa Mafunzo kwa Maafisa TEHAMA ni utaratibu endelevu ndani ya Mamlaka, tunajitahidi kila mwaka tuwe na mafunzo jumuishi pamoja na mafunzo maalumu (specific) katika maeneo mbalimbali ya TEHAMA na malengo yetu ni kuzifikia taasisi zote za Umma." alisema.

Aidha, Bw.Ricco aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia elimu waliyoipata katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ili kuboresha huduma za serikali mtandao nchini na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Washiriki wa mafunzo hayo walieleza kuridhishwa na utaratibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, wa kutoa mafunzo mbalimbali yanayolenga kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA ili kuwasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao yalianza Novemba 21 mwaka huu ambapo mada mbalimbali katika maeneo ya Uchambuzi wa Mifumo ya TEHAMA, Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA, Miongozo, Viwango, Usimamizi, Ubora na Usalama wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini zilitolewa.

**PICHANI: Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA e-GA Bw.Ricco Boma, akifafanua jambo wakati akifunga mafunzo ya siku sita kwa Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka katika taasisi mbalimbali za umma, yaliyotolewa na e-GA mwishoni mwa mwezi Novemba 2023, jijini Dodoma.**





> Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ipo tayari kushirikiana na taasisi za uchukuzi katika kushauri na kujenga mifumo mbalimbali ya TEHAMA, itakayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika sekta ya usafirishaji na kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi

Bw.Godfrey Masanja
Meneja wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA (e-GA)

# SEKTA YA USAFIRISHAJI YASHAURIWA KUBUNI MIFUMO YA TEHAMA YENYE TIJA

**e-GA itaendelea kusisitiza matumizi ya TEHAMA serikalini kwa kuzingatia Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha yanaleta tija kwa taifa na wananchi kwa ujumla.**

Meneja wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw.Godfrey Masanja, amewashauri wadau wa usafirishaji nchini, kubuni mifumo ya TEHAMA inayoendana na mazingira ya kibiashara ili kuleta tija kwenye taasisi zao.

Masanja alitoa wito huo, wakati alipowasilisha mada kuhusu Sheria na Huduma za Serikali Mtandao, kwenye mkutano wa 16 wa Wadau wa Usafirishaji uliofanyika tarehe 07 Desemba, 2023 jijini Arusha.

Alifafanua kuwa, kwa sasa dunia inashuhudia ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma kwa wananchi, hivyo taasisi za usafirishaji hazina budi kusanifu mifumo inayoboresha huduma hizo ili kwenda sambamba na mazingira ya kibiashara yaliyopo katika sekta hiyo.

"Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ipo tayari kushirikiana na taasisi za uchukuzi katika kushauri na kujenga mifumo mbalimbali ya TEHAMA, itakayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika sekta ya usafirishaji na , upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi", alisema Masanja.

Aliongeza kuwa, e-GA itaendelea kusimamia matumizi ya TEHAMA serikalini kwa kuzingatia Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha yanaleta tija kwa taifa na wananchi kwa ujumla.

Mkutano huo uliandaliwa na Wizara ya Uchukuzi na kuhudhuriwa na Maafisa kutoka katika Taasisi na Mamlaka mbalimbali za usafirishaji nchini, huku e-GA ikiwa ni miongoni mwa wadhamini wa mkutano huo.







**Baadhi ya wadau wa Sekta ya Uchukuzi wakifuatilia mada mbalimbali kwenye kongamano la 16 la wadau wa Sekta ya Uchukuzi lililofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 05 hadi 08 mwezi Disemba 2023.**

# MATUKIO KATIKA PICHA

**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi cheti cha shukran ya udhamini Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao ( e-GA) Bw. Ricco Boma, kwenye Mkutano Mkuu wa 7 wa Mashirika ya Utangazaji ya Umma Kusini mwa Afrika (SABA). Mkutano huo ulifanyika kwa siku tatu kuanzia Oktoba 10 hadi 12, 2023 katika ukumbi wa Hoteli ya Golden Tulip Kisiwani Unguja ambapo e-GA ilikuwa ni miongoni mwa wadhamini wa mkutano huo.**





**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, akizindua Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Watu wenye Ulemavu Nchini (PD-MIS).Lengo la Mfumo huo ni kukusanya, kuhifadhi na kuchakata taarifa za Watu wenye Ulemavu, ikiwemo taarifa za aina ya ulemavu walizonazo, taarifa za wazazi/walezi wao, ngazi za elimu, shughuli za kiuchumi wanazoshughulika nazo n.k. Pia, mfumo huo unaisaidia Serikali kufahamu mahitaji muhimu ya watu wenye ulemavu, ili kuweza kuwapatia huduma stahiki ikiwemo vifaa saidizi, huduma za afya, huduma za kisheria, ujuzi, stadi kazi, ajira na elimu, ili kuhakikisha kuwa, watu wenye ulemavu wanaweza kujitegemea na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.Mfumo huo umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ulizinduliwa tarehe 2 Disemba,2023 jijini Dodoma.**










Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (katikati,mstari wa mbele) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh.George Simbachawene (wa pili kushoto,mstari wa mbele) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi kutoka taasisi mbambali za Umma ,baada ya uzinduzi na makabidhiano ya Mfumo wa Kieletroniki wa kuratibu Ununuzi wa Mafuta Serikalini (GIMIS) uliofanyika tarehe 21 Oktoba,2023.




Baadhi ya viongozi kutoka Taasisi mbalimbali za Umma akiwemo Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba (katikati), wakishuhudua uzunduzi wa mfumo wa GIMIS uliozinduliwa na Waziri wa Fedha Dkt.Mwigulu Nchemba katika ukumbi wa Kambarage, ofisi za Hazina Jijini Dodoma.



**Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh. Ridhiwani Kikwete ((Mb), akiongea na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao e-GA) kituo cha Iringa wakati alipotembelea ofisi hizo tarehe 20 Novemba ,2023 ili kukagua utendaji kazi wa Mamlaka katika kituo hicho.**

**Mhe. Kikwete ameridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka, na kuwataka watumishi wake kuendeleza ubunifu wa Mifumo ya TEHAMA inayotatua changamoto zilizopo nchini pamoja na kuwa wazalendo kwa maslahi mapana ya Taifa.**





**Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh.Ridhiwani Kikwete (Kushoto ),akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mh. Benedict Ndomba (Wa pili kushoto) kuhusu eneo ambalo e-GA inatarajia kujenga ofisi mkoani Iringa.**



*"Karibu tuijenge Serikali Kidijitali"*

**Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA Bw. Ricco Boma pamoja na Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Sultana Seiff, wakishiriki mjadala kuhusu Teknolojia zinazoibuka na namna zinavyowezakutumika katika kuleta mabadiliko ya dijiti na fursa za ajira, kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, katika Kongamano la saba (7) la TEHAMA lililofanyika Oktba 18 - 20, 2023 katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.**








**Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka taasisi mbalimbali za Serikali wakiwa kwenye Mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao. Mafunzo yaliratibiwa na e-GA yalifanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 21 hadi 26,Novemba 2023.**










## Viongozi mbalimbali watembelea banda la e-GA katika maonyesho ya tatu ya Kidijitali ya Afya na Ubunifu, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kampasi ya Mloganzila,Dar es Salaam.




**Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe.Nape Nnauye (Mb), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao Dkt. Jaha Mvulla, kuhusu bunifu mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kupitia kituo hicho.**




**Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel, akipokea maelezo kutoka kwa Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao, Dkt. Jaha Mvulla, wakati alipotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika maonesho ya tatu (3) ya Kidigitali ya Afya na Ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).**




**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi Dkt.Faustine Ndugulile (Mb),akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao Dkt. Jaha Mvulla, kAuhusu bunifu mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kupitia kituo hicho.**

**Maafisa wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakitoa elimu kwa washiriki mbalimbali waliotembelea banda la e-GA kwenye maonesho ya tatu ya kidigitali ya Afya na Ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.**












# MATANGAZO


RESEARCH, INNOVATION & DEVELOPMENT CENTER (RIDC)
We are providing Internship and Volunteering positions
Application is Open.
You can apply through Ubunifu Portal
https://ubunifu.ega.go.tz/
Get Industrial Experience in:
- Software Development
- Blockchain Technology
- Internet of Things (IOT)
- Artificial Intelligence (AI)
- Machine Learning (ML)
- Electronics & Embeded Systems
- Cyber Security
- Data Science
- & Others


Click or Scan Here to Register
The 4th e-Government Annual Meeting
Theme
"Ensuring Compliance to e-Government Policies, Laws,Standards and Guidelines for Secure Electronic Data Exchange"
06 - 08 February 2024
Arusha International Conference Center
Participation Fee TZS 450,000/=
Register through https://www.tsms.ega.go.tz
0764 292 299 / 0763 292 299
Participants
Accounting Officers, Board Members, Head of ICTs, ICT Officers, Procurement Officers, Auditors, Human Resource Officers, Communication Officers,Planning Officers, Accountants and Other ICT beneficiaries.

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE

Salum Mussa
Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

Hamis Ali
Meneja Ukaguzi wa Ndani

Rafael Rutaihiwa
Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai
Meneja wa Huduma kwa Wateja

## MHARIRI MKUU

Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI


Catherine Peter | Afisa Habari
Queenter Mawinda | Afisa Habari

## WAPIGA PICHA

Mussa Enock |Afisa Habari
Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA

Edgar Msamba | Afisa TEHAMA




Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mtandao.
S.L.P. 2833, 40404 DODOMA.
+255 026 - 296 1957
www.ega.go.tz
info@ega.go.tz
barua@ega.go.tz